**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI

## KIKAO CHA NANE

**08 FEBRUARI, 2018**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI

## KIKAO CHA NANE – TAREHE 08 FEBRUARI, 2018

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI MKUU:**

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ya Mwaka 2016.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa mwaka 2017.

## III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

## IV. MASWALI YA KAWAIDA:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**99. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mradi wa maji wa Hydom umechukua muda mrefu kumalizika na Wananchi wanasubiri maji huku muda wa Mkataba na Mkandarasi ukiwa umeisha:-

Je, kwa nini Serikali isimfukuze Mkandarasi huyo.

## OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

### 100. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, ni nini mikakati ya dhati ya Serikali katika kunusuru na kuzuia uchafuzi wa mazingira ya Mto Rubana ambao unaingiza maji yake katika Ziwa Victoria na ni chanzo kikubwa cha maji katika Vijiji vya Tingrima, Kyandege, Mugeta, Mariwanda, Sarakwa, Kihumbu na Hungari katika Jimbo la Bunda.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

### 101. MHESHIMIWA MWANTUMU DAU HAJI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Kumekuwa na sintofahamu ya matumizi ya ardhi pamoja na masharti maalum yanayotakiwa katika mapori yetu hususan kwa wawekezaji na Wananchi wanaozunguka hifadhi na mapori tengefu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo hili.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**102. MHESHIMIWA HAMAD SALIM MAALIM (KOJANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 16 inatoa uhuru wa faragha kwa raia:-

Je, kwa nini Jeshi la Polisi linapokwenda kupekua kwenye nyumba yenye mume na mke hutumia Askari wa kiume peke yao.

## WIZARA YA MADINI:

**103. MHESHIMIWA ANNA JORAM GIDARYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:- Mgodi wa Tanzanite ulioko Mererani Wilaya ya Simanjiro ni mgodi wenye idadi kubwa ya vijana wanaofanya kazi katika mgodi huo na kumekuwa na historia ya matukio ya maafa kila mwaka ya vifo vya watu wengi:-

(a) Je, Serikali imefanya utafiti gani ili kubaini chanzo cha maafa hayo yanayolikumba Taifa kila mwaka na kusababisha kupoteza nguvu kazi ya Taifa letu;

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha utaratibu maalum kwa wamiliki wa vitalu vya Tanzanite kuwalipa kifuta jasho wahanga wote wanaopatwa na maafa wanapokuwa kazini.

**WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:**

**104. MHESHIMIWA DEOGRATIAS FRANCIS NGALAWA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji:- Miradi ya Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga imekuwa ikizungumzwa na Serikali kwa Awamu zote; na katika Awamu hii ya Tano imewekwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016 - 2021):-

(a) Je, ni lini miradi hiyo itaanza;

(b) Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa Wananchi wa Mundindi na Nkomang’ombe waliotoa maeneo yao kupisha miradi hiyo.

## WIZARA YA NISHATI:

### 105. MHESHIMIWA NEEMA WILLIAM MGAYA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Ni muda mrefu tangu *transformer* katika Kijiji cha Itengelo Kata ya Saja imefungwa lakini umeme haujawashwa:-

Je, ni lini Serikali itawasha umeme katika Kijiji hicho.

## WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

### 106. MHESHIMIWA JUMA ALI JUMA (DIMANI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Kuna mgogoro wa Ardhi kati ya Jeshi na Wananchi wa Kisakasa hali inayoleta wasiwasi kwa Wananchi:-

(a) Je, ni lini Serikali itaupatia ufumbuzi mgogoro huo;

(b) Je, kwa nini Serikali isiwaruhusu Wananchi hao kuendelea na shughuli zao za kilimo na mifugo wakati wakisubiri ufumbuzi wa tatizo hilo.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**107. MHESHIMIWA LATHIFA HASSAN CHANDE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Halmashauri ya Mji wa Liwale imetumia takribani shilingi milioni 540 katika ujenzi wa mradi wa umwagiliaji katika Kata ya Mtawango lakini mradi huo umejengwa chini ya kiwango na hakuna thamani ya matumizi ya fedha *(value for money):-*

Je, Serikali ipo tayari kwenda kukagua mradi huo na kufanya uchunguzi ili kubaini kasoro za mradi huo na kuwawajibisha wote watakaobainika kuuhujumu.

## V. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2017.

**DODOMA** **S.N. KAGAIGAI**
**08 FEBRUARI, 2018** **KATIBU WA BUNGE**